

TAARIFA YA IDARA YA ELIMU YA SEKONDARI KWA AJILI YA TOVUTI YA HALMASHAURI

1. UTANGULIZI

Idara ya Elimu ya Sekondari ni moja ya idara za Halmashauri ya Wilaya ya Masasi. Idara hii ilianzishwa mwaka **2009** baada ya Serikali kugatua usimamizi na uendeshaji wa shule za sekondari kutoka kwenye Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis kwenda na kusimamiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa (Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Majiji).

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ina Jumla ya shule za sekondari **27**, kati ya hizo shule **26** ni za Serikali na shule **1** ni ya mtu binafsi. Kati ya shule za Serikali **26**, shule **23** ni shule za kutwa na shule **3** ni shule za bweni ikiwa mojawapo ni shule ya kidato cha tano na sita. Jumla ya wanafunzi wa shule za sekondari za Serikali ni **7293** wakiwemo wavulana **3965** na wasichana **3,328** na shule ya binafsi ina jumla ya wanafunzi wavulana **501**. Halmashauri ina jumla ya wanafunzi kwa shule zote za Serikali na binafsi **7794** wakiwemo wavulana **4466** na wasichana **3328**.

2. DIRA NA MWELEKEO

2.1 DIRA, DHIMA NA MALENGO YA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA 2014

Msingi wa elimu na mafunzo utajikita katika kumjenjea Mtanzania misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi, umahiri na kumwezesha kujitegemea. Elimu ya kujitegemea itaendelea kuongoza utoaji wa elimu na mafunzo kwa

kuzingatia mabadiliko yanayotokea katika jamii, kisiasa, kiuchumi, kisayansi na kiteknolojia.

2.1.1 **DIRA**

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa.

2.1.2 **DHIMA**

Kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa letu.

2.2 **LENGO LA JUMLA LA SERA YA ELIMU NA MAFUNZO**

Kuwa na Watanzania walioelimika na wenye maarifa na ujuzi kuweza kuchangia kwa haraka katika maendeleo ya Taifa na kuhimili ushindani.

3. **ELIMU YA SEKONDARI**

3.1 **MATAMKO YA SERA KUHUSU ELIMU YA SEKONDARI**

3.1.1 **SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 1995**

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 ilifafanua kuwe Elimu ya Sekondari ina maana ya Programu (Mpango) kamili wa elimu

inayotolewa kulingana na Mitaala ya Serikali na kupatikana kwa wanafunzi ambao watakuwa wamemaliza elimu ya msingi.

Nchini Tanzania elimu rasmi ya shule za Sekondari ina ngazi mbili. Ngazi ya kwanza ni elimu ya sekondari ya Ngazi ya Kawaida ya miaka minne, ambapo ngazi ya pili ni Programu ya Miaka miwili ya elimu ya Sekondari ya ngazi ya Juu. Ngazi ya kawaida huanzia kidato cha I na kuishia kidato cha 4, wakati Ngazi ya Juu ina kidato cha 5 mpaka cha 6

3.1.2 SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 imerekebisha muda wa elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali ili kuleta tija, ufanisi na matumizi bora ya rasilimali

TAMKO

- 3.1.2.1 Serikali itaweka utaratibu wa elimu ya awali kuwa ya lazima na kutolewa kwa watoto wenyewe umri kati ya miaka mitatu hadi mitano kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja.
- 3.1.2.2 Serikali itaweka utaratibu wa elimumsingi kuwa ya lazima kuanzia darasa la kwanza hadi kidato ha nne; na kutolewa kwa miaka kumi na umri wa kwanza darasa la kwanza kuwa kati ya miaka minne hadi sita kulingana na maendeleo na uwezo wa mtoto kumudu masomo katika ngazi husika.

- 3.1.2.3 Serikali itaweka utaratibu wa kuhakikisha muda wa kukamilisha elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali za elimu baada ya elimumsingi unalenga mwanafunzi kupata ujuzi stahiki kulingana na Mfumo wa Tuzo wa Taifa.
- 3.1.2.4 Serikali itahakikisha kuwa elimumsingi katika mfumo wa umma inatolewa bila ada.

4. LENGO LA IDARA

Kutoa nafasi ya upataji maarifa, ujuzi na kuelewa ili wanafunzi wajiunge na taasisi za ufundi na mafunzo ya kitaalamu ya elimu ya juu.

5. VITENGO VILIVYOPO KATIKA IDARA

Idara ya elimu ya sekondari ina jumla ya vitengo viwili (**3**) ambavyo hufanya shughuli zake kwa ushirikiano na kumsaidia mkuu wa idara ambaye ni msimamizi mkuu wa shughuli za idara katika kuleta matokeo tarajiwa. Vitengo vya idara ni pamoja na kitengo cha Taaluma kinachosimamiwa na Afisa Elimu Taaluma Wilaya, kitengo cha Vifaa na Takwimu kinachosimamiwa na Afisa Elimu Vifaa na Takwimu Wilaya na kitengo cha ufundi kinachosimamiwa na Afisa Ufundi wa Wilaya na vyote vikiwa chini ya mkuu wa idara ambaye ni Afisa Elimu Sekondari wa Wilaya.

5.1 MAJUKUMU YA VITENGO

5.1.1MAJUKUMU YA AFISA ELIMU TAALUMA (W)

- Kusimamia masuala yahusuyo maendeleo ya taaluma na michezo katika shule za sekondari wilayani.

5.1.2MAJUKUMU YA AFISA ELIMU VIFAA NA TAKWIMU (W)

- Kukusanya kuchambua na kuunganisha takwimu mbalimbali zinazohusu elimu ya sekondari.


5.1.3MAJUKUMU YA AFISA ELIMU UFUNDI

- Kusimamia upanuzi wa elimu ya sekondari kusimamia ujenzi wa majengo mapya katika shule za zamani au katika kuanzisha Shule mpya.

6. MUUNDO WA IDARA

Idara imeundwa na ngazi tano. Ngazi ya Wilaya kuna mkuu wa idara ambaye ni Afisa Elimu Sekondari Wilaya. Idarani kuna maafisa wa vitengo vitatu ambavyo ni:- Afisa Elimu Taaluma (W), Afisa Elimu Vifaa na Takwimu (W) na Afisa Elimu Ufundi (W). Ngazi ya kata wapo Waratibu Elimu Kata wakifuatiwa na wakuu wa shule pamoja na walimu na watumishi wao katika ngazi ya Shule.

Muundo wa idara



7. MIONGOZO NA SERA ZINAZOTUMIWA NA IDARA

Katika kutekeleza shughuli zake, idara inatumia Sera na Miongozo mbalimbali inayotolewa na serikali katika kusimamia utoaji wa elimu. Sera na miongozo hiyo ni kama ifuatavyo:-

1. Sera za Elimu na Mafunzo ya mwaka **2014**.
2. Sheria ya Elimu ya mwaka **1978** na marekebisho yake.
3. Miongozo mbalimbali ya elimu
4. Nyaraka mbalimbali za elimu
5. Maagizo mbalimbali ya Serikali

8. MAJUKUMU YA IDARA

Majukumu ya idara ni pamoja na:-

- Kuiwakilisha Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia katika ngazi zote kuhusu masuala ya elimu ya sekondari.
- Kufafanua na kusimamia utekelezaji wa Sera za Elimu na Mafunzo kwa kufuata miongozo na taratibu, sheria na kanuni zinazoongoza utoaji wa elimu ya sekondari, katika shule za serikali na zisizo na serikali
- Kusimamia masuala yahusuyo maendeleo ya taaluma na michezo katika shule za sekondari wilayani.
- Kuwa mshauri wa masuala ya elimu sekondari katika Wilaya.
- Kusimamia upanuzi wa elimu ya sekondari.
- Kushughulikia masuala ya mitihani ya ndani na nje katika usimamizi na uratibu.
- Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mipango ya elimu ya sekondari

- Kusimamia na kuratibu masuala yanayohusu kuinua ubora wa mazingira ya kujifunzia na kufundishia.
- Kudhibiti na kusimamia nidhamu ya walimu na wanafunzi wa shule za sekondari katika Halmashauri.
- Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa Shule na kufuatilia utekelezaji wa taarifa za ukaguzi wa shule za sekondari zilizokaguliwa na uthibiti ubora wa Shule.
- Kupanga walimu wa sekondari kulingana na mahitaji ya kila shule wilayani
- Kusimamia haki na maslahi ya walimu na wanafunzi wa sekondari.
- Kukusanya, kuchambua na kuunganisha takwimu mbalimbali zinazohusu elimu ya sekondari.
- Kufanya ufuutiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo

9. HUDUMA ZINAZOTOLEWA NA IDARA MARA KWA MARA

Nia kuu ya idara ya elimu ya sekondari ni kutoa huduma kwa walimu, wanafunzi na wananchi kwa ujumla kuhusu masuala ya elimu ya sekondari, huduma hizo ni kama ifutavyo;:-

- Kusimamia utoaji wa elimu ya sekondari shulenii(Kufuatilia Ufundishaji na ujifunzaji).
- Kutoa ushauri wa kitaalamu wa elimu ya sekondari katika ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na maeneo mengine.
- Ufuutiliaji wa miradi ya ujenzi shulenii.
- Kuwahudumia wananchi, wazazi, walezi, walimu na wanafunzi katika masuala yahusuyo elimu ya sekondari.

10. TAARIFA ZA WATUMISHI

Jumla ya watumishi wote wa idara ya elimu ya sekondari ni watumishi 441 wakiwamo watumishi wa idarani 8, watumishi walimu 394 wakiwemo wanaume 315 na wanawake 79, waratibu elimu kata 10 na watumishi wasio walimu 29.

Jedwali namba 1: Watumishi wa idara ya elimu ya sekondari na namba zao za simu

Na	JINA	JINSI	CHEO	NAMBA YA SIMU
1	Bi.Paula .A. Nkane	KE	Afisa Elimu Sekondari (W)	0713-882658 0787-882658
2	Bw. Juma .S. Bushiri	ME	Afisa Elimu Taaluma (W)	0784-635351
3	Bw. Shabani Kinyongo	ME	Afisa Elimu Vifaa na Takwimu(W)	0752-788621
4	Bw. Richard .C. Makota	ME	Afisa Elimu Vifaa na Takwimu(W)	0784-794992
5	Bw. Vitalis Chinguile	ME	Afisa Elimu Ufundii(W)	0784593476
6	Bi. Hawana Hatibu	KE	Mpiga chapa/katibu muhtasi	0654677466
7	Bw. Valentino Mahurua	ME	Mhudumu	0657474124
8	Bi. Suzan Mkanda	KE	Mtunza Kumbukumbu	0767306408

Jedwali namba 2: Orodha ya shule na majina ya wakuu wa shule na namba zao za simu

Na	Namba ya usajili	Jina la shule	Kata shule ilipo	Kijiji shule Ilipo	Jina la Mkuu wa shule	Namba ya simu
1	S.1869	NAMALENGA	NAMALENGA	MKANGAULA	JAMALI MBUMILE	0787778883
2	S.639	LUKULEDI	LUKULEDI	LUKULEDI	KUDRA SIMBA	0787045965
3	S.3962	CHIWATA	CHIWATA	CHIWATA	KASSIM MZEE	0755750280
4	S.1219	MBEMBA	CHIGUGU	CHIGUGU	GEOFREY NTANDU	0784226155
5	S.3965	SINDANO	SINDANO	LUATALA	YONA MWEMI	0789046235
6	S.3966	CHANIKANGUO	MPINDIMBI	MPINDIMBI	HUMPHREY R. AMLIMA	0786004868
7	S1849	ISDORE SHIRIMA	CHIKUKWE	MANDIWA	CLAUDIUS Y. LUPAPA	0715886363
8	S.1217	MAKONGONDA	MAKON'GONDA	MAKON'GONDA	MOHAMEDI NAHOCHI	0786331866
9	S.1867	LULINDI	LULINDI	LULINDI	FRANK FINIUS	0756339803
10	S.2372	NAMAJANI	NAMAJANI	NAMAJANI	HOSEA IGHIMBI	0783956532
11	S.1316	MWENA	NDANDA	NJENGA	RASHIDI NAMCHAMBE	0783120881
12	S.1866	NANJOTA	NANJOTA	NANJOTA	BENEDICT MNALI	0784534325
13	S.1890	LUPASO	LUPASO	LUPASO	CRISPIN RICHARD	0785597040
14	S.3964	NAMWANGA	MKUNDI	MKOLOPOLA	HAMZA NAMPOTO	0782587458
15	S.1862	NANGANGA	NANGANGA	NANGANGA	ROBERT MLENGULE	0712532285
16	S.4549	NANGOO	NANGOO	MDENGA	BRUNO F KAPINGA	0784278359
17	S.1108	CHIUNGUTWA	CHIUNGUTWA	CHIUNGUTWA	MAURIDI CHIDWA	0784738391
18	S.1868	NAMOMBWE	MCHAURU	NAMOMBWE	EDULAI CHAULA	0784727929
19	S.602	NDWIKA	LULINDI	NDWIKA CHINI	PAULINE NDOMBA	0683369102
20	S.105	CHIDYA	CHIWATA	CHIDYA	ZAWADI MDIMBE	0628698028
21	S.3059	MKALAPA	CHIKUNDI	MKALAPA	KHARIDI MTEREMKO	0755307258
22	S.3055	MKULULU	MKULULU	CHINGOLUPI	AKRAM MOHAMED	0782408765
23	S.3054	MBUYUNI	MBUYUNI	MBUYUNI	KARIMU LIWOWA	0784225547
24	S.3062	NAMATUTWE	NAMATUTWE	CHINGULUNGULU	FADHILI MLAPONI	0786825021
25	S.25	NDANDA	NDANDA	MPOWORA	MOREGA MONGATE	0688469670
26	S.3961	CHIWALE	CHIWALE	CHIWALE	MOHAMEDI MBOTELA	0626333110
27	S.3209	ABBEY	MWENA	MWENA	FR.AUGUSTINO OMBEI	0784371612

11. MAENDELEO YA KITAALUMA

11.1 HALI YA UFAULU

Halmashauri ya Wilaya ya Masasi ina jumla ya Shule za Sekondari **26** ambazo wanafunzi wake walifanya mitihani ya kumaliza Elimu ya Sekondari kidato cha Pili na Nne kwa miaka ya 2014, 2015 na 2016. Halmashauri pia inayo Shule ya Sekondari ya kidato cha tano na sita ambayo wanafunzi wake walifanya mitihani ya taifa kidato cha Sita kwa miaka ya 2014, 2015, na 2016.

Matokeo ya Mitihani hiyo yanaonyeshwa hapo chini:-

11.1.1 MATOKEO YA MTIHANI WA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI MWAKA 2014 HADI 2016

Jedwali i: Taarifa ya Matokeo ya Mtihani wa Upimaji Kidato cha Pili kwa Miaka 2014, 2015, na 2016

MWAKA	WALIOAN DIKISHWA	WALIO FANYA	WALIO FAULU	% YA UFAULU	WALIO FELI	% YA WALIOFELI	Nafasi kimkoa	Nafasi kitaifa
2014	1397	1283	1181	96	45	4		
2015	1473	1341	1028	77	313	23	2/6	137/160
2016	2224	2098	1420	68	678	32	2/6	161/167

11.1.2 MATOKEO YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA NNE MWAKA 2014 HADI 2016

Jedwali iii: Taarifa ya Matokeo ya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne kwa Miaka 2014, 2015, 2016

MWAKA	WALIOANDI KISHWA	WALIO FANYA	WALIO FAULU	% YA UFAULU	WALIO FELI	% YA WALIOFELI	Nafasi kimkoa	Nafasi kitaifa
2014	800	798	514	67	255	33	4/7	110/169
2015	1430	1421	806	57	496	43	2/6	101/168
2016	1148	1137	738	65	399	35	2/6	100/178

11.1.3 MATOKEO YA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA SITA MWAKA 2014 HADI 2016

Jedwali v: Taarifa ya Matokeo ya Kidato cha Sita kwa Miaka 2014, 2015, na 2016

MWAKA	WALIOANDI KISHWA	WALIO FANYA	WALIO FAULU	% YA UFAULU	WALIO FELI	% YA WALI OFELI	Nafasi kimkoa	Nafasi kitaifa
2014	382	380	372	97	5	3	4/5	225/268
2015	424	421	417	99	4	1	3/4	182/265
2016	553	545	541	99	4	1		

12. MIUNDOMBINU NA SAMANI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI

Hali ya Miundombinu na samani katika shule za sekondari ni kama ifuatavyo:-

Na	AINA	MAHITAJI	ILIOPO	UPUNGUFU	% YA UPUNGUFU
1	Vyumba vya madarasa	216	235	0	0
2	Nyumba za walimu	394	150	244	62
3	Majengo ya utawala	26	12	14	54
4	Maktaba	26	3	23	88
5	Maabara za fizikia	26	26	0	0
6	Maabara za kemia	26	26	0	0
7	Maabara za baiolojia	26	26	0	0
8	Mabweni na Hostel	39	31	8	21
9	Jiko	26	4	22	84
10	Stoo	52	11	41	79
11	Bwalo	26	4	22	84
12	Vyoo kwa walimu	60	50	10	17
13	Vyoo kwa wanafunzi	336	364	0	0
14	Meza za wanafunzi	7293	7649	0	0
15	Viti vya wanafunzi	7293	7421	0	0
16	Meza za walimu	394	221	173	44
17	Viti vya walimu	394	274	120	30
18	kabati	245	69	176	72
19	Shelfu	208	76	132	63
20	Vitanda	1131	1072	59	5

11. **MAWASILIANO YA IDARA**

Kwa mawasiliano, maswali na maelekezo idara inatumia njia zifuatazo; -

1. Sanduku la barua – Idara ya Elimu Sekondari Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji(W)

S.L.P. 60 MASASI- MTWARA

2. Barua pepe (e-mail address) – deos.masasidc@gmail.com
3. Namba za simu - Simu: 2510031
4. Fax: 2510031

NB: Unaweza pia kuwasiliana na maafisa wa idara kuitia namba zao katika simu za mkononi kama zilivyotolewa hapo juu.

